



021 FORM THREE - MIDTERM EXAMINATION - MARCH 2026 BUMBULI DC - FORM THREE - MIDTERM EXAMINATION - MARCH 2026 BUMBULI DC
 MUDA: SAA 3 KISWAHILI MACHU 2026

MsomiBora.com

- SEHEMU A (ALAMA 16)

- Page 1 of 4

viii. Waimbaji wote watasafiri kesho mchana " sehemu ya kiarifu iliyopigiwa mstari inabeba dhana gani kisarufi?

- A. Chagizo
- B. Shamirisho.
- C. Prediketa.
- D.kijalizo.
- E.kishazi huru.

ix. Baada ya mkuu wako kukuteua kushiriki shindano la uandishi wa insha wilaya inahusisha mwanafunzi mmoja kutoka katika kila shule ,kwa lengo la kupata mwanafunzi mmoja atakaekwenda kushiriki mashindano ya uandishi wa insha kitaifa huko mkoani tabora .Utazigatia mmbo gani muhimu ya uandishi wa insha kati ya haya yafuatayo:-

- A. Lugha za kisanaa,alama za uandishi,na mwandiko nadhifu tu.
- B. Kichwa cha habari,mwandiko nadhifu na mpangilio wa mawazo tu.
- C. Kichwa cha habari ,alama za uandishi na kiini kizuri cha insha .
- D. Kichwa cha habari,utangulizi mzuri ,kiini cha insha ,mwisho wa insha na taraibu zote za uandishi.
- E. Lugha ya kisanaa,kichwa cha habari, upangaji wa mawazo katika aya na mwandiko nadhifu.

x. "Tupia mzigo fasta ngoma inang'oa nanga hiyo" mtindo huu wa lugha unaweza kutumiwa katika mandhari ya :-

- A. Kiwandani.
- B. Kituo cha polisi.
- C. Bandarini.
- D. soko kuu.
- E. Mgodini

2. Oanisha herufi ya jibu sahihi kutoka orodha B na kipendele cha swali kutoa orodha A kwa kuandika herufi husika .

ORODHA A	ORODHA B
i.mtajo	A.Hutumika mwanzoni mwa sentensi
ii. nukta pacha	B. Hutumika mwanzoni mwa jina lolote.
iii. Mkato.	C. Hutumika kuonesha nukuu ya maneno.
iv. mabano	D. Hutumika katika kuorodhesha vitu.
v. Herufi kubwa.	E. Hutumika kutenga dakika
vi. Kistari	F Hutumika kuonesha maelezo ya ziada.
	G Hutumika mwishoni mwa sentensi kuonesha kuwa neno linaendelea
	H .Hutumika kugenga wazo moja na jingine.
	I. Hutumika kuonesha pumziko katika sentensi ndefu.

SEHEMU B (ALAMA 54)

3. a) Miongoni mwa dhima kuu ya viambishi tamati katika shina au mzizi wa kitenzi ni kubadili kitenzi kuwa Nomino thibitisha kauli hii kwa kubadili vitenzi vifuatavyo kuwa nomino ukitumia kiambishi (-o).

- i. Cheza.
- ii. Imba.
- iii. Andika.
- iv. Sema.
- v. Itika.

(b) Mwalimu wako wa kiswahili kidato cha kwanza alikueleza kuwa sifa mojawapo ya aina yamaneno ni kuwa : kila aina ya neno linaweza kubadilika kuwa aina yoyote ya neno kutegemea na matumizi au mpangilio wa neno husika katika tungo . Kwa kuthibitisha ukweli wa mwalimu wako ,tunga zenye kutumia maneno na maelekezo uliyopewa katika kipengele kwa hivi vifuatavyo:-

- i. Neno" Musa" litumike kama kivumishi.
- ii. Neno" Alikuwa litumike kama kitenzi kishirikishi
- iii. Neno " Tuma" litumike kama Nomino.
- iv. Neno" watano" litumike kama kiwakilishi

4. a) Upatanisho wa kisarufi huwa na lengo la kuifanya sentensi iwe/ziwe fasaha. Panga maneno yafuatayo katika ngeli zake kisha tunga sentensi.
- Kalamu
 - Chai
 - Uji
 - Mkutano
 - Ugonjwa
- b) Matumizizi ya kiimbo husaidia kubainisha lengo la mzungumzaji katika sentensi. Bainisha lengo la kiimbo katika sentensi zifuatazo:
- Mwanafunzi anasoma kwa bidii.
 - Mwanafunzi, akisoma kwa bidii atafaulu
 - Mwanafunzi anasoma kwa bidii?
 - Mwanafunzi anasoma kwa bidii!
5. a) Tunga sentensi kubainisha matumizi yafuatayo ya mofimu "KI"
- Masharti
 - Kundelea Kwa tendo.
 - Kitenzi kishirikishi
 - Upatanisho wa kisarufi.
- b) Kwa kila sentensi oneshwa kiima na kiarifu Kwa kutenga na kuandika "K" kwa kiima na "A" Kwa kiarifu.
- Rais wa Tanzania alikuwa anahutubia wananchi.
 - Ng'ombe wangu mkubwa amekula majani yote.
 - Mtoto wangu amekunywa maji machafu.
 - Mwizi aliyeikamatwa jana ameachiwa.
 - Wanafunzi watoro walipewa adhabu
6. Tunga sentensi zenye miundo ifuatayo:-
- N + T + E
 - N + U + N + T
 - N + T + N
 - N + U + N + T + N
 - N + V + t + N
 - Hs + N + V + TS + TS + TS + T
7. Taja methali unazoweza kutumia kuadilisha watu wenye tabia zifuatazo:
- mtu mwenye tabia ya wizi.
 - mtu asiyejali jeraha dogo mwilini mwake .
 - mtu anayerukia magari na hakubali ushauri wa katazo la anachokifanya.
 - Mtu mwenye bidii katika kazi.
 - Mtu mvumilivu.
 - Mtu mwenye dharau.

8. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata.

1. Badilisha mtazamo, yaache ya kukariri,
Maisha yabadilika, wakati wawa ukuta,
Kazi yataka ujuzi, vyeti using'ang'anie,
Hapa kazi ndio, mbiu sije jisahaulisha
2. Agizo uzingatie, acha randa randa ovyo
Tumia ujuzi wako, zao la elimu yako,
Kazi fanya kwa bidi, upate mradi wako,
Siku zote zingatia, kujua ndio kuishi.
3. Siangalie ya ndugu, wala Jirani mzee,
Yeye ajira lipata, kwa hizo zama za chuma,
Zama zimepinduliwa, hilo weka akilini,
Tumia ujuzi wako, upate wako mradi.
4. Lako puto ukishika, madhila hukuambaa,
Kuku wa John kuibwa, wewe kando utakuwa,
Hayakusumbui nafsi, moyo wako utaubwaga,
Usikose zingatia, ujuzi kipaumbelei.

Maswali:

- a) Shairi hili linahusu nini?
- b) Pendekeza kichwa kinachofaa kwa shairi
- c) Taja mawazo makuu matatu yanayopatikana katika shairi ulilosoma
- d) Ni ujumbe gani unaupata katika shairi hili?
- e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi
 - i) Randaranda
 - ii) Kipaumbele

SEHEMU C (ALAMA 30)

Jibu maswali mawili kutoka katika sehemu hii swali la **tisa 9 ni lazima**

9. Wafanyabiashara Hodari hutunza fedha zao benki. Wanafasihi Hodari pia hutunza kazi zao kwa ajili ya vizazi vijavyo. Wewe kama mwanafasihi nguli, kwa hoja sita (6) fafania namna utakavyotunza kazi za fasihi simulizi.
10. Rafiki yako kipenzi Siwema Limpopo anatarajia kuadhimisha sherehe ya kuzaliwa kwake tarehe 05/04/2026 nyumbani kwao mji mwema na na agependa rafiki zake wote wahudhurie lakini hajui kuandika kadi ya mwaliko. Ukiwa mbobezi katika kuandika kadi za mialiko, msaidie rafiki yako Siwema kuandika kadi ya mwaliko ili kufanikisha sherehe yake.
11. Bwana Shekallaghe analalamika kuwa Bwana Juma anadai kuwa hakuna ulazima wa kuendelea kutumia vitabu vya kamusi shuleni kwa kuwa tuko dunia ya sayansi na teknolojia ,hivyo mambo yote yanafanyika mtandaoni .Ugana na bwana Juma kumwelimisha bwana shekallaghe kuhusu umuhimu wa matumizi ya kamusi kwa wanafunzi walioko shuleni.toa hoja sita (6) tu.